# SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI YA MWAKA WA 2020

TIME FOR NATURE



## MWONGOZO

**kwa watu binafsi, makundi ya kidini, mashirika ya biashara, miji, serikali, shule na vyuo, makundi ya vijana na mashirika ya uraia**

WORLD ENVIRONMENT DAY

UN environment programme

COLOMBIA 2020

# MWONGOZO WA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI

TIME FOR NATURE

**Kauli mbiu ya Siku ya Mazingira Duniani, tarehe 5 mwezi wa Juni mwaka wa 2020 ni bayoanuai — wito wa kuchukua hatua kukabiliana na kupungua kwa kasi kwa spishi na uharibifu wa dunia asilia. Takribani aina milioni 1 ya mimea na wanyama wanaweza kuangamia kabisa kutoka katika sayari, haswa kutokana na shughuli za binadamu. Mwenyeji wa Siku ya Mazingira Duniani ni Kolombia kwa Ushirikiano na Ujerumani. Siku ya Mazingira Duniani inatupa fursa ya kutafakari kuhusu jinsi ambavyo mifumo yetu ya uchumi imebadilika na athari yake kwa mazingira. Dunia haipaswi kupuuza masuala haya wakati huu tunapokabiliana na janga la virusi vya korona na changamoto za hali ya hewa. Kolombia ni mojawapo ya nchi iliyo na aina mbalimbali ya spishi duniani. Ikiwa ni pamoja na aina 3,500 ya mimea ya jamii ya okidi, asilimia 19 ya aina zote za ndege duniani na kadhalika. Serikali zimetoa kipao mbele kwa utunzaji wa bayoanwai.**


**Tovuti ya Siku ya Mazingira Duniani inatoa taarifa kuhusu jinsi ya kujisajili, shughuli zainazoendelezwa mtandaoni, ajenda na live feeds.**

# BAYOANUAI NI NINI NA INA UMUHIMU GANI?

Bayoanuai, au uanwai wa viumbe, ni aina mbalimbali ya viumbe wanaopatikana duniani. Hii ni pamoja na takribani aina milioni 8 ya viumbe wanaopatikana kwenye sayari-ikiwa ni pamoja na mimea, wanyama, kuvu na bakteria – mifumo ya ekolojia inayotumika kama makazi yake – kama vile bahari, misitu, mazingira ya maeneo ya milima na matumbawe- pamoja na uanuai wa kimaumbile.

Mifumo dhabiti ya ekolojia, iliyo na bayoanuai ya kutosha, ni muhimu kwa maisha ya binadamu. Mifumo ya ekolojia huwezesha maisha kupitia njia mbalimbali: husafisha hewa yetu, husafisha maji yetu, huhakikisha tunapata lishe bora, hutupa madawa ya kiasili na vifaa vya kutumia kutengeneza madawa na hupunguza uwezekano wa majanga kutokea.

Lakini hatujayatunza mazingira. Tunashuhudia mioto ya ajabu nchini Brazil, mjini California na nchini Australia. Pia, kuna uvamizi wa nzige katika eneo la Pembe ya Afrika na kuangamia kwa matumbawe. Janga la virusi vya korona linaloendelea– mojawapo ya magonjwa yaliyotokea hivi karibuni yanayozuka kutoka kwa wanyama – ni kiashiria kuwa kuna uhusiano kati ya ubora wa sayari na afya yetu.



# KUNA HATARI IPI?

Spishi milioni moja ya mimea na wanyama ziko hatarini kuangamia– baadhi yake katika kipindi cha miongo – kwa mjibu wa ripoti ya hivi karibuni iliyotolewa na Jukwa la Kimataifa la Sayansi la Kuhudumia Bayoanuai na Mifumo ya Ekolojia (**IPBES**). Kila spishi ina umuhimu wake wa kuboresha na kudumisha mifumo mizuri ya ekolojia. Uharibifu wa bayoanuai na wa maeneo ya makazi unaweza kuongeza uwezekano wa kusambaa kwa magonjwa ambukizi na virusi.

Uchumi wa kimataifa una uhusiano mkubwa na bayoanuai. Huduma zinazotokana na bayoanuai zinakadiriwa kuwa kati ya dola za Marekani trilioni 125 na na trilioni 140. Chakula tunachokula, hewa tunayopumua, maji tunayokunywa hutoka kwa mazingira. Tunapokaribia kufikia bilioni 10 kwenye sayari, tunapaswa kuchukua fursa zilizopo na kuyathamini mazingira asilia na wala tusiyadhuru.

**Habari njema** ni kuwa tunaweza kukabiliana na uharibifu wa bayoanuai kwa **kubadili mienendo yetu** kwa mazingira na **kuchukua hatua** za kuwajibika zaidi ili kuyatunza. Ni sharti tutunze na kuhifadhi makazi ya wanyamapori, kubadilisha jinsi tunavyozalisha na kutumia bidhaa, kukuza miundo msingi inayojali mazingira na kubadili chumi ili zishughulikie mazingira.

Jinsi dunia inavyokabiliana na janga la virusi vya COVID-19 ni ishara kuwa tukiwajibika mapema na kushirikiana tutakabiliana na masuala nyeti yanayoathiri jamii zetu. Nchi zinapoweka mikakati ya kujiimarisha, ni muhimu kuyafanya mazingira nguzo ya maamuzi yetu kwa manufaa ya watu na kwa manufaa ya sayari.

**“Bayoanuai –nguzo ya maisha duniani – inaendelea kudidimia kote ulimwenguni, huku uwezo wa mazingira kuwezesha binadamu kuishi vizuri ukididimia . Hali hii hatari ni tishio kwa chumi, kipato, upatikanaji wa chakula cha kutosha na ubora wa kiwango cha maisha ya binadamu kote ulimwenguni kwa mjibu wa ripoti nne kuu zilizoandikwa na zaidi ya wataalamu wakuu 550 kutoka pembe zote za dunia.”**

**Jukwa la Kimataifa la Sayansi la Kuhudumia Bayoanuai na Mifumo ya Ekolojia (ya mwaka wa 2019)**

# NI NINI KINACHOSABABISHA UHARIBIFU WA BAYOANUAI?

Mambo matano makuu yanayosababisha uharibifu wa bayoanuai kama yanavyojitokeza kwa ripoti ya hivi karibuni iliyotolewa na **IPBES** na **GEO-6** yanatokana na sughuli za binadamu. Uharibifu wa bayoanuai unaweza kuzuiliwa kwa kubadilisha bidhaa tunazotumia, kubadilisha jinsi tunavyozalisha na kwa kutunza mazingira. Kutunga sera dhabiti za mazingira na kuchukua hatua za uwajibikaji vitasaidia kubadili mienendo yetu.

### MABADILIKO KATIKA MATUMIZI YA ARDHI

Hitaji la chakula na rasimali linatupelekea kukata miti, linasababisha mabadiliko katika matumizi ya ardhi na kuharibu maeneo asilia ya makazi kote ulimwenguni. Asilimia ishirini na sita ya ardhi isiyo na theluji hutumiwa kulisha mifugo na asilimia 33 ya mimea ni lishe kwa mifugo. Sasa, theluthi moja ya mchanga wenye rutuba umeharibiwa na asidi, uchafuzi na matumizi mengine mabaya ya ardhi.

### MATUMIZI MABAYA YA MIMEA NA WANYAMA

Matumizi mabaya ya mimea na wanyama yanayofanywa na binadamu ikiwa ni pamoja na uvuvi, ukataji wa miti na uwindaji haramu wa wanyamapori ni tishio kwa maisha ya viumbe wadogowadogo na wakubwawakubwa; kuanzia kwa wanyamapori maarufu kama vile kakakuona, ambaye ndiye huuzwa zaidi kimagendo duniani, hadi kwa samaki aina ya beluga anayeuzwa bei ghali kutokana na mayai yake. Umasikini unaweza kufanya watu kujihusisha na uwindaji haramu na ukataji wa miti kinyume cha sheria. Maendeleo yasiyojali uendelevu hupelekea unyakuzi wa maeneo ya makaazi ya wanyamapori na kusababisha mahitaji ya bidhaa kutokana na wanyamapori.

### UDHARURA WA KUSHUGHULIKIA MABADILIKO YA TABIA NCHI

Mabadiliko ya tabia nchi na kuongezeka kwa hali mbaya ya hewa ni chanzo cha uharibifu wa makazi na uharibifu wa ardhi. Kwa mfano ongezeko la joto baharini linafanya theluji kuyeyuka; theluji ni muhimu kwa maisha ya dubu wa maeneo baridi, kwa wanyama wa baharini wenye manyoya mazuri na kwa ndege wavuwao. Umwagaji wa asidi baharini husababisha kuchuchuka kwa matumbawe. Inakadiriwa kuwa kufikia mwa kwa 2050, moja kati ya kila aina nne ya spishi zitaangamia kabisa iwapo hali itaendelea jinsi ilivyo.

### UCHAFUZI

Uchafuzi ni tishio kubwa kwa bayoanuai na husababisha madhara mabaya kwa maji safi na makazi ya maeneo ya bahari. Kuna uwezekano wa kuwa na vijipande vidogovidogo vya plastiki na uchafu wa plastiki unaoelea baharini. Hii ni kati ya asilimia 60 na asimia 90 ya uchafu wote baharini. Utupaji wa taka kiholelaholela huathiri mimea na wanyama, huku kemikali za kuua wadudu, mbolea na kemikali zingineno zikidhuru vichavushaji kama vile nyuki na popo, ambavyo hukabiliana na wadudu.

### SPISHI HATARI ZA KIGENI

Spishi hatari za kigeni ni tishio kwa sababu huvamia au kushindana na viumbe na kubadili makazi, husababisha uzalishaji mtambuka na spishi za kiasili na kusababisha magonjwa. Utandawazi huongeza uwezo wa viumbe kusafiri na hata kusababisha viumbe wageni katika maeneo ambayo hayana viumbe hao kupitia kwa biashara na utalii. Hali hii huathiri jamii husika na makazi.

# UHARIBIFU WA BAYOANUAI NA COVID-19

Wakati wa Siku ya Mazingira Duniani, **wengi wanaposalia majumbani,** tutafakari jinsi tulivyojikuta katika hali hii.

Janga la COVID-19 ni ukumbusho tosha kuwa maisha ya binadamu hutegemea hali ya sayari. Virusi vya korona vinatokana na wanyama, kumainisha kuwa huwa vinasambazwa kutoka kwa wanyama hadi kwa binadamu. Utafiti unaonyesha kuwa magonjwa ya aina hii yanaendelea kuongezeka. Kwa sasa, karibu watu bilioni 1 huambukizwa magonjwa kutoka kwa wanyama na mamilioni hufariki kila mwaka. Asilimia sitini ya magonjwa yote yanayotambulika hutoka kwa wanyama, kama ilivyo na asilimia 75 ya magonjwa yote ambukizi yanayozuka.

Wanasayansi wanatabiri kuwa tusipobadili mienendo yetu kwa maeneo ya makazi ya wanyama, tuko hatarini zaidi kuambukizwa magonjwa ya virusi. Kuzuia uwezekano wa magonjwa ambukizi kutokea siku zijazo, ni sharti tukabiliane na matishio kwa mifumo ya ekolojia na kwa wanyamapori, ikijumuisha uharibifu wa maeneo ya makazi na unyakuzi wa ameneo hayo. Pia, tukabiliane na biashara haramu, uchafuzi, spishi hatari za kigeni na ongezeko la mabadiliko ya tabianchi.

Siku ya Mazingira Duniani inanuia kumfanya kila mtu kusikika - wananchi wanapaswa kushurutisha serikali zao kutekeleza ahadi walizotoa za kutunza mazingira, kukomesha uchafuzi na kuhakisha kuwa sheria za mazingira zinatekelezwa. Kampuni zinapaswa kubuni mifumo endelevu ya usambasaji, ikiwa ni pamoja na kufanya kilimo na kuunda bidhaa kwa njia isiyodhuru mazingira. Wananchi na mashirika ya uraia watafute mbinu za kuhifadhi na kuboresha mifumo ya ekolojia iliyoharibika. Na watumiaji wa bidhaa watafakari kabla ya kuvinunua. Tukibadili mienendo yetu, tunaweza kuungana na kutafuta njia ya kuishi vizuri kati yetu na kuishi vizuri na mazingira.

**Ni wakati wa #KutunzaMazingira**

**Siku ya Mazingira Duniani, Ni wakati wa #KutunzaMazingira. Ni wakati wa kubadili mienendo yetu kwa mazingira. Ni wakati wa kutoa kipao mbele kwa mazingira wakati wa kufanya uamuzi. Tunafahamu tunachohitaji ili kuishi vizuri na mazingira.**

**Je, tutatoa kipao mbele kwa makazi yetu na kuyasikiliza?**

# JINSI TUNAVYOTAKA UTUSAIDIYE

**Mwongozo huu una sehemu tatu: jifundishe, shiriki na chukua hatua. Ni muhimu kwa sababu watu wengi huenda wamejitenga kutokana na janga la COVID-19. Unachohitaji ili kushiriki ni intaneti, kitabu au hata kuwa mbunifu tu.**

### JIFUNZE:

Kutotoka nyumbani ni fursa nzuri ya kupata mafunzo zaidi kuhusu spishi za wanyamapori na makazi yake tunayotumia pamoja duniani. Kutotoka nyumbani kunaweza kukupa fursa ya kutafakari kuhusu mazingira na umuhimu wake maishani mwetu na jinsi tunaweza kuhamasisha ili kupata matokeo chanya.

### SHIRIKI:

Tunapoelekea Siku ya Mazingira Duniani, itakayojiri tarehe 5 mwezi wa Juni, UNEP itaanzisha msururu wa mawasiliano kupitia mitandao ya kijamii kwa lugha nane. Tutakuuliza utueleze kwa nini ni wakati wa #KutunzaMazingira. Hii inatoa fursa kwako kushiriki nasi kwa nini unapenda dunia asilia, kwa serikali kuonyesha juhudi zake za kutunza mazingira na kwa mashirika mbalimbali kufanya uhamasishaji.

### CHUKUA HATUA:

Baada ya tarehe 5 mwezi wa Juni kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Mazingira wa Umoja wa Mataifa mwaka wa 2021 – wakati ambapo mawaziri wa mazingira wataainisha mambo ya kushughulikiwa kwa dharura ulimwenguni – tunatoa wito kwenu wote muanze kuchukua hatua kutokana na maarifa mliopata ili kusaidia kukomesha uharibifu wa bayoanuai na mabadiliko ya tabianchi. Ni kwa kufanya tu tunayohitaji kufanya ndipo mazingira yatakapoanza kuimarika na kuhakikishia watu wote hatima bora iliyoimarika.

# MTU BINAFSI ANAWEZA KUFANYA NINI?



**Kila mmoja wetu ana wajibu wa kutekeleza ili kukomesha uharibifu wa bayoanuai na kutunza mazingira kwa manufaa ya binadamu. Kama watu binafsi, ni sharti tutafakari kabla ya kununua na kutumia bidhaa ndiposa tufanye uamuzi unaofaa. Tubadili mienendo yetu ya uharibifu na kuwa watunzaji wa mazingira, mwanzo, ni sharti TUJIFUNZE kuhusu tunachoweza kufanya; SHIRIKI maarifa hayo na familia na marafiki zetu wakati wa Siku ya Mazingira Duniani na baadaye; na KUCHUKUA HATUA zitakazoleta mabadiliko.**

**Hapa kuna rasilimali muhimu unazoweza kutumia KUJIFUNZA kuhusu jinsi unavyoweza kutunza mazingira:**

- Jifahamishe kuhusu kile serikali na mji wako hufanya ili kutunza mazingira
- Jiunge na "Earth School" na ushiriki katika vipindi 30 kuhusu mazingira vinavyoendeshwa na TED-Ed vilivyoundwa na walimu maarufu wa mazingira duniani ted.ed.com/Earth-School
- Jifundishe kuhusu jinsi unavyoweza kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kupitia kwa kampeni ya Umoja wa Mataifa ya Chukua Hatua Sasa un.org/en/actnow/
- Jifundishe kuhusu uchafu wa plastiki na unavyoathiri viumbe wa baharini kupitia kampeni ya UNEP ya Bahari Safi - cleanseas.org/
- Jifundishe kuhusu ulanguzi wa spishi zilizo hatarini kuangamia zinazouzwa kimagendo kupitia biashara haramu ya wanyamapori wildfor.life/the-campaign
- Pitia "Anatomy of Action", inayoorodhesha baadhi ya mambo ambayo mtu binafsi anaweza kufanya kupunguza uzalishaji wa gesi ya ukaa anatomyofaction.org
- Jisajili kupitia iNaturalist, jamii ya mtandaoni ya wanaasilia, ambapo unaweza kutoa matokeo ya utafiti wako kuhusu mimea na wanyama, kukutana na wapenda mazingira wenzako, na kufanya uchunguzi kuhusu masuala ya mazingira
- Jifundishe kuhusu pengo lililosalia kuwezesha nchi kudhibiti joto duniani kuwa nyusi joto 1.5. unenvironment.org/interactive/emissions-gap-report/2019/
- The Nature Conservancy ni shirika lisilokuwa la kibiashara linalofanya kazi kuhakikisha watu na mazingira vinaimarika
- Soma ripoti kuhusu matumizi ya ardhi, haki za ardhi na athari zake kwa mazingira catalogue.unccd.int/823_GLO_Full_Report_ENG.pdf catalogue.unccd.int/825_Transformative_action_brochure%20GM.pdf catalogue.unccd.int/1210_UNCCD_SPI_2019_Report_1.2.pdf
- Jifahamishe zaidi kuhusu Mkataba wa Kimataifa wa Utunzaji wa Mimea hapa, pitia mwongozo huu ili ufahamu jinsi unavyoweza kuzungumzia masuala haya, na utumie rasilimali hii kwenye mitandao ya kijamii
- Fahamu iwapo vipodozi vyako vina vipande vidogovidogo vya shanga hatari kupitia kwa apu ya "Beat the Microbead app" beatthemicrobead.org/download-the-beat-the-microbead-app-and-take-part-in-ocean-conservation/
- IUCN's #NatureforAll Discovery Zone wana vifaa vinavyoweza kutumiwa kwa ubunifu – vinajumuisha video, maandalizi ya vipindi na vitabu vya futuhi - vya kukusaidia kujifundisha kuhusu mazingira

**Hapa kuna namna unavyoweza KUSHIRIKI ujumbe huu wakati wa Siku ya Mazingira Duniani:**

- Zuru mitandao ya jamii ya UNEP kwenye sehemu ya 'feeds' kwanzia tarehe 28 mwezi wa Mei hadi tarehe 5 mwezi wa Juni na ushiriki na ulimwengu umuhimu wa kutunza mazingira. Hakikisha unatumia tagi, #TutunzeMazingira na #SikuYaMazingiraDuniani
- Tagi watu kadhaa/mashirika/kampuni unapojibu maswali na uwaombe washiriki kwenye majadiliano
- CITIES4FORESTS wamezindua Shindano la Misitu. Shiriki kwenye shindano na upande mti cities4forests.com/forest-challenge/
- Wasilinaa kwa njia inayoeleweka kwa urahisi kwa kuhakikisha kuwa unatumia rasilimali za kuaminika ili kuepuka kutoa ujumbe usiokuwa wa kweli.

**Hapa kuna yale unayoweza kufanya ili KUCHUKUA HATUA zitakazonufaisha mazingira:**

- Badili chakula unachokula ili ujumuishe vyakula vinavyojali mazingira, hasa vya protini
- Punguza safari - Punguza safari wakati tutakaporudia hali ya kawaida baada ya janga la korona
- Wacha maeneo usiolima kwenye bustani yako kama eneo la makazi kwa vichavushaji na wadudu.
- Fahamisha miji na serikali yako umuhimu wa kutekelezea ahadi za mazingira walizozitoa
- Epuka kununua plastiki zinazotumika tu mara moja. Uchafuzi wa plastiki kwa mazingira huaminiwa kimakosa kuwa chakula na wanyama, wanaoishi kwenye ardhi na waishio baharini. Aina nyingi ya spishi, huweza kudhurika vibaya na hata kufa
- Tumia bidhaa mara nyingi iwezekanavyo
- Jiundie bustani ya kisasa kwenye balkoni yako au shiriki katika kusaidia jamii kuunda bustani za kisasa mijini kwa kutumia mimea ya kiasili inayootesha maua
- Punguza matumizi ya kemikali zinazoweza kuongeza sumu mchangani na kwenye maji yapatikanayo chini ya ardhi nyumbani. Badala yake, tumia bidhaa za kiasili, kama siki na sabuni zisizokuwa na kemikali na maji
- Tenga eneo la kutupa uchafu kwenye bustani yako na tumia kama mbolea na upande mimea yako mwenyewe kwenye bustani au kwenye sanduku la kuoteshea mimea dirishani.
- Fanya utafiti kuhusu jinsi ya kununua bidhaa na vyakula vilivyooteshwa karibu na wewe.

# VIONGOZI WA DINI NA MAKUNDI YA KIDINI YANAWEZA KUFANYA NINI?



**Makundi ya kidini yana jukumu la kutekeleza ili kukomesha uharibifu wa bayoanuai na kutunza mazingira kwa manufaa ya binadamu. Viongozi wa kidini wa ngazi zote wanaweza kushawishi waumini kuishi vizuri duniani na kutafuta ajira zisizochafua mazingira. Mwanzo, tunapaswa** KUJIFUNZA **kuhusu kile tunachoweza kufanya;** KUSHIRIKI **maarifa hayo na wanajamii wakati wa Siku ya Mazingira Duniani, na ikiwezekana** KUCHUKUA HATUA **za kubadili tunachostahili kubadili.**

**Hapa kuna baadhi ya rasilimali kwa makundi ya kidini ili KUJIFUNZA kuhusu vile yanavyoweza kutunza mazingira:**

- Mradi wa UNEP wa 'Faith for Earth Initiative' unalenga kushawishi na kushirikisha mashirika ya kidini ili kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu na kufikia Ajenda ya mwaka wa 2030 unenvironment.org/about-un-environment/faith-earth-initiative/religions-and-environmental-protection

- Jukwa la 'Yale Forum' la dini na ekolojia lina makitaba inayotoa rasilimali kuhusiana na dini mbalimbali na mafundisho yake kuhusu mazingira fore.yale.edu/search/node/biodiversity

- Laudato Si, Waraka wa Pili wa Baba Mtakatifu, Papa Francis unaonyesha hali ya kusikitisha kutokana na uharibifu wa mazingira na ongezeko la joto duniani www.vatican.va/content/francesco/en/encyclicals/documents/papa-francesco_20150524_enciclica-laudato-si.html

- Mwongozo wa kufundishia watoto wa Uislamu na Mazingira husaidia kufundisha watoto na kuwapa mazoezi yanayojumuisha kazi rahisi wanazoweza kufanya na mazoezi ya ubunifu issuu.com/lutfiomar/docs/teachers-guide_body_v3

- Pia, unaweza kupata rasilimali za Mafundisho ya Dini ya Uyahudi kuhusu mazingira ikiwa ni pamoja na shughuli, majadiliano na mpangilio wa vipindi kwa Aytzim, shirika la kushughulikia mazingira lisilokuwa la serikali aytzim.org/resources/educational-materials

- Jarida la 'Human Responsibility and the Environment' huandikwa kwa kuzingatia mafundisho ya dini ya Hindu digitalcommons.butler.edu/cgi/viewcontent.cgi?article=1077&context=jhcs

- Mchango wa jamii ya Sikh kwa 'UNDP/Alliance of Religions and Conservation Plans', unalenga kusaidia dini kuu duniani kupitia utamaduni wake kuboresha uhusiano wake na mazingira na unaweza kupatikana hapa arcworld.org/downloads/Sikh-EcoSikh-Seedplan-5YP.pdf

**Hapa kuna ushauri jinsi ambavyo unaweza SHIRIKI ujumbe huo wakati wa Siku ya Mazingira Duniani:**

- Endesha ibada, maandiko, mjadala na majadiliano ya aina hii mtandaoni huku ukisisitiza vifungu kutoka kwa vitabu vya dini vinavyosisitiza utunzaji wa mazingira

- Shiriki makala ya kidini yanayohusu mazingira kwenye mitandao ya jamii na kutagi makundi mengine ya kidini ili yafuate nyayo

- Andaa hafla ya kuchanga pesa za kutumia kwa shughuli za mazingira mahali unakotoka ili kuwezesha waumini kushiriki

- Sisitiza kuhusu mabadiliko mtakayofanyia mahali pa kuabudia ili kuwezesha uendelevu wakati watu watakapoanza kurudi katika maeneo yao ya ibada na uwahimize waumini kufanya vivyo hivyo

- Shiriki taarifa kuhusiana na janga la COVID-19 na uonyeshe uhusiano wake na uharibifu wa bayoanuai ili kukabiliana na taarifa zisizo za kweli

- Shirikiana na shirika la kijamii linalozalisha nishati jadidifu ili kuwezesha waumini kununua kwa bei nafuu na kuwashawishi kununua

- Shirikiana na duka la jumla lililo karibu nawe ili ukusanye vyakula vinavyoelekea kuharibika na kuwapa maskini bila malipo.

**Hapa kuna yale unayoweza kufanya ili KUCHUKUA HATUA za kushughulikia mazingira:**

- Himiza kuwa na mafunzo kuhusu utunzaji wa bayoanuai wakati wa maombi

- Badilisha maeneo ya ibada kwa kujali mazingira na kuyafanya ya kudumu, ili kuweka mfano wa kuigwa na jamii

- Wakati wa mafundisho ya kidini, jadili kuhusu umuhimu wa kutunza bayoanuai, na kukabiliana na madhara mabaya kwa mazingira na kwa uchumi

- Kuza utamaduni wa lishe bora, ikiwa ni pamoja na kupunguza ulaji wa nyama na kuhimiza ulaji wa vyakula vinginevyo endelevu

- Kuza maeneo yaliyohifadhiwa yanayomilikiwa na mashirika ya kidini

- Mashirika ya kidini na taasisi za kidini humiliki asilimia 5 ya misitu inayotumika kufanya biashara duniani, himiza kuwepo na mienendo ya kudumu ya kuhifadhi na kutunza misitu

- Himiza watu kupanda miti wakati wanapokusanyika

- Sambaza miche ya kiasili kwa waumini wakati wanapokusanyika kwa ibada

- Tenga taka na utumie ile inayoweza kutumika kuunda mbolea

- Shiriki katika mijadala na makongamano yanayohusu mazingira yanayoandaliwa na serikali na mashirika ya kimataifa

- Sisitiza umuhimu wa “kujiimarisha” baada ya COVID-19 huku mazingira yakipewa kipao mbele wakati wa kufanya uamuzi

- Hamasisha watu zaidi washirikiane ili kupunguza uharibifu na kutumia chakula kidogo

# MASHIRIKA YA BIASHARA



**Sekta ya binafsi ina jukumu la kutekeleza katika kukabiliana na uharibifu wa bayoanuai na kuhifadhi mali ghafi. Mashirika ya biashara hutegemea kupata vifaa vya uzalishaji na vya kutumia katika mchakato wa uundaji wa bidhaa. Yanaweza kutumia mbinu thabiti na endelevu katika mfumo mzima wa usambasaji ili kukomesha uharibifu unaoendelea na kuanza kutunza mazingira Ni sharti tuanze na KUJIFUNZA kuhusu kile tunachoweza kufanya; KUSHIRIKI maarifa hayo na jamii wakati wa Siku ya Mazingira Duniani na baadaye; na KUCHUKUA HATUA za kuleta mabadiliko tunayohitaji.**

**Hapa kuna baadhi ya rasilimali zinazoweza kutumiwa na mashirika ya biashara ili KUJIFUNZA kuhusu jinsi yanavyoweza kutunza mazingira:**

- 'Global Compact' ni makubaliano ya Umoja wa Mataifa yasiyokuwa ya lazima yanayohimiza mashirika ya biashara kote duniani kuunda sera za kudumu na za kijamii, na kutoa taarifa kuhusiana na utekelezaji wake unglobalcompact.org

- Jukwa la 'One Planet Network' ni la kujitolea kwa jamii za kimataifa ili kuharakisha uzalishaji na utumiaji wa bidhaa kwa njia endelevu katika nchi zilizoendelea na zile zinazoendelea oneplanetnetwork.org

- Rasilimali za UNEP za Kushirikisha Sekta ya Binafsi ni pamoja na mikakati, ripoti na habari za kweli

- Ripoti ya UNEP ya 2019 Global Status Report for Buildings and the Construction Sector inaonyesha wazalishaji wakuu wa kaboniksidi katika sekta ya ujenzi

- Taarifa kuhusu mashirika ya biashara kutoka kwa GEO zinalenga kutoa kwa jamii ya wafanyabiashiara sayansi kutoka kwa 'UNEP's Global Environment Outlook' ili kuleta mabadiliko yanayohitajika kubuni uchumi usiochafua mazingira na kuunda bidhaa zinazotumiwa tu mara moja. Biashara Bora, Dunia Bora, ripoti ya Kamisheni ya Wafanyabiashara inaainisha mambo yanayoweza kufanywa na mashirika makuu ya biashara ili kuwezesha dunia kuwa endelevu, isiyo na ubaguzi inapoendelea. report.businesscommission.org/report

- OECD- 'Private Sector Peer Learning Policy Brief' inangalia mabadiliko ya tabianchi na mbinu za kukuza biashira zisizochafua mazingira oecd.org/dac/peer-reviews/Policy-Brief-4-Private-Sector-Engagement-to-Address-Climate-Change-and-Promote-Green-Growth.pdf

- Jifahamishe zaidi kuhusu 'International Plant Protection Convention' hapa; pitia mwongozo huu ili kupata ushauri wa jinsi ya kuwasiliana kuhusu masuala haya; na tumia rasilimali hizi kwa mitandao ya jamii

- Soma ripoti hizi kuhusu matumizi ya ardhi, haki za ardhi na athari zake kwa mazingira catalogue.unccd.int/823_GLO_Full_Report_ENG.pdf catalogue.unccd.int/825_Transformative_action_brochure%20GM.pdf catalogue.unccd.int/1210_UNCCD_SPI_2019_Report_1.2.pdf

- Pitia rasilimali hizi kujifunza kuhusu jinzi ya kutunza ardhi ili isiharibike catalogue.unccd.int/1210_UNCCD_SPI_2019_Report_1.2.pdf https://knowledge.unccd.int/drought-toolbox

- Jifundishe kuhusu matumizi mazuri ya ardhi kupitia podcast na knowledge tool vilivyoanzishwa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kukabiliana na Majangwa

- Ripoti ya Kamisheni ya Ulaya inachunguza jinsi ya kushughulikia mazingira vizuri katika sekta ya chakula na ya vinywaji ec.europa.eu/jrc/en/publication/eur-scientific-and-technical-research-reports/best-environmental-management-practice-food-and-beverage-manufacturing-sector

**Hapa kuna mambo ambayo mashirika ya biashara yanaweza kufanya ili KUSHIRIKI jumbe wakati wa Siku ya Mazingira Duniani:**

- Anzisha mradi mpya, weka malemgo mapya, au chukua hatua za kuleta mabadiliko zitakazoboresha mazingira, na na weka utaratibu wa jinsi ya kuyafikia
- Toa wito ili watu watume mawazo ya ubunifu ya kuleta mabadiliko kwenye sekta yako ya biashara ili kujali mazingira zaidi
- Jiunge na CEO Carbon Neutral Challenge
- Panga kujiunga na muungano kama vile Business for Nature, unaotoa wito wa kukabiliana na uharibifu wa bayoanuai
- Komesha matumizi ya plastiki zinazotumika tu mara moja kwenye kampuni yako katika ngazi ya uzalishaji na usambasaji wa bidhaa kwenye mtandao kisha tagi mashirika mengine ya biashara
- Unda mikakati mipya ya kupunguza uharibifu wa chakula na kabiliana na uzalishaji wa gesi ya ukaa
- Iwapo wewe ni mfanyabiashara mwanamitindo, shawishi watu kutumia rangi ya kiasili na vipande vya kiasili vya nguo kupitia vitu unavyotengeneza
- Ongeza rangi ya kijani kwenye shirika lako kwa kupanda miti na maua ili kupunguza joto na kuboresha bayoanuai
- Himiza wafanyakazi wako na wateja wako washiriki katika Siku ya Mazingira Duniani kwa kuuliza kuhusu maoni yao kuhusu jinsi shirika lako linavyoweza kuboresha na kutunza mazingira

**Hapa kuna baadhi ya rasilimali zinazoweza kutumiwa na mashirika ya biashara KUCHUKUA HATUA za kutunza mazingira:**

- Elewa, thamini na uonyeshe jinsi unavyotegemea mazingira na jinsi unavyoyaathiri
- Iwapo shirika lako linahitaji mali ghafi, itafute vizuri kwa kutafuta cheti kutoka kwa Tume ya Usimaizi wa Msitu (FSC), B Corp au Rainforest Alliance Certified
- Saidia serikali kuwekeza kwenye usimamizi wa ardhi iliyo na maji ili kuboresha hali na kiwango cha maji ili kunufaisha watu na mifumo ya ekolojia
- Anzisha mifumo ya masoko ya kaboni, kwa mfano kuruhusu wakulima kushiriki katika soko la kaboni kwa hiari ili waweze kutuzwa kwa kutumia mbinu za utunzaji wa mazingira kama vile kupanda mimea bila kulima na kupanda mimea inayozuia mmomonyoko wa udongo

- Kufanya uwekezaji na shughuli zinazoweza kusaidia kuimarisha bayoanuai na kuzuia uharibifu wake
- Komesha ukataji wa miti na zuia kufanya makazi ya kiasili kuwa maeneo ya uzalishaji
- Hakikisha unapata kikamilifu manufaa yanayotokana na huduma za mifumo ya ekolojia na faida inayotokana na shughuli za biashiara
- Hakikisha uendelevu hata wakati wa kuweka mikakati
- Tafuta jinsi ya kuzalisha, kusambaza, kutumia bidhaa na kutumia rasimali kikamilifu. Punguza uzalishaji wa gesi ya ukaa na epukana na kemikali hatari zinazodhuru bayoanuai
- Tumia vifaa visivyochafua mazingira kama taka kutoka mitoni, vifaa vilivyotengenezwa kutoka kwa vitu vya kudumu na vifaa vidogovidogo vya kujengea vinavyotumia nishati ya jua na kuzuia joto
- Nunua kutoka kwa soko lililo karibu na wewe ili kukuza biashara vya eneo hilo, na ikiwezekana nunua kutoka kwa wakulima wanaojali mazingira
- Wekeza kwenye utafiti na kwa uundaji wa teknolojia ya kisasa inayojali mazingira katika kampuni yako
- Mwongozo wa Biashara wa Umoja wa Mataifa ni fursa kwa sekta ya binafsi ili kuweza kuchangia na kuimarisha juhudi wakati wa kukabiliana na janga hili
- ‘UN Global Compact’ imebuni jukwaa la kutumiwa na CEOs kurekodi video kuhusu jinsi kampuni zao zinavyokabiliana na COVID-19 (CEOs Taking Action)

# MIJI INAWEZA KUFANYA NINI?



**Siku hizi, watu wengi huishi mijini na kutumia takribani asilimia 75 ya rasilimali zinazotokana na mazingira. Kufikia mwaka wa 2050, UN inakadiria kuwa asilimia 80 ya idadi ya watu duniani wataishi mijini. Kwa hivyo, miji ina jukumu kubwa la kutekeleza ili kutunza rasilimali zilizopo duniani na kuhudumia watu. Ili kukomesha uharibifu unaoendelea na kuanza kutunza mazingira zaidi, ni sharti tuanze na; KUJIFUNZA kuhusu yale tunayoweza kufanya; KUSHIRIKI maarifa hayo na wananchi wakati wa Siku ya Mazingira Duniani; na KUCHUKUA HATUA za kubadilisha yale tunayostahili kubadilisha.**

**Hapa kuna rasilimali zinazoweza kutumiwa na meya wa miji, na manispaa KUJIFUNZA jinsi wanavyoweza kutunza bayoanuai:**

- Miongozo ya UNEP huonyesha njia za kutumia mazingira na rasilimali vizuri na kikamilifu unenvironment.org/news-and-stories/story/new-neighborhood-creating-new-community-around-sustainability-and-social
- Ripoti ya UNEP inatathmini jinsi ambavyo miji inaweza kuwa endelevu na jinsi inavyoweza kutumia rasimali kikamilifu wakati idadi ya watu inapoongezeka katika maeneo ya mjini sustainabledevelopment.un.org/content/documents/1124SustainableResourceEfficientCities.pdf
- Ripoti ya UNEP GEO Cities Report hutoa taarifa za kuaminika zilizosasishwa kwa serikali, kwa wanasayanyi, kwa waunda sera na kwa umma kuhusu jinsi ya kuboresha upangaji na uendashaji wa mazingira ya mjini
- Ripoti hii ya UNEP huonyesha jinsi serikali za mtaa na uamuzi zinaofanya unaweza kusaidia kuboresha hali ya mazingira duniani
- The Cities and Biodiversity Outlook inatoa muhtasari wa jinsi miji inavyoathiri bayoanuai na kutathmini njia kumi zinazoweza kutumiwa na miji kuimarisha uhifadhi wa mazingira na kutumia mali ghafi kwa njia endelevu
- Pitia rasilimali hizi kujifunza jinsi ya kuzuia uharibifu wa ardhi catalogue.unccd.int/1210_UNCCD_SPI_2019_Report_1.2.pdf knowledge.unccd.int/drought-toolbox
- Mwongozo wa UN Habitat Guidelines unaonyesha jinsi ya kufanya maendeleo kwa kushirikisha miji na maeneo ya mashambani
- CitiesWithNature, mradi unaoendelezwa na ICLEI, IUCN na The Nature Conservancy, ni jukwaa linalotumiwa na miji na wabia kujadiliana na kushirikiana citieswithnature.org/what-is-citieswithnature/
- Mradi wa 'Nature of Cities' huandaa majadiliano kuhusu masuhuhisho ya mjini kwa changamoto za mazingira www.thenatureofcities.com/
- 'Cities4Forests' huhimiza miji kushirikiana, kuhifadhi, kushughulikia na kuboresha misitu iliyo karibu cities4forests.com/
- Jifundishe jinsi ya kushughulikia mazingira katika maeneo ya mjini kupitia rasilimali hizi: citieswithnature.org/ cbc.iclei.org/una-handbook-series/ cbc.iclei.org/value-nature-urban-life/


**Hapa kuna ushauri unaohusu jinsi miji inavyoweza KUSHIRIKI ujumbe huu wakati wa Siku ya Mazingira Duniani**:

- Jiunge na mradi wa CitiesWithNature unaotambua umuhimu wa mazingira na kuyaimarisha katika miji na vitongoji vyake
- Jisajili na kikundi cha C40 Cities Climate Leadership Group
- Amua kubuni 'green area' katika mji wako
- Tumia akaunti za mitandao ya jamii kusisitiza kuhusu bayoanuai ya kiasili inayopatikana katika mji wako na nini kipo hatarini kuangamia iwapo hatua hazitachukuliwa
- Tumia wananchi mbegu za kiasili wakati wa Siku ya Mazingira Duniani wanazoweza kpanda kwenye balkoni zao au bustanini ili kuwezesha bayoanuai kuwepo
- Jiunge na Climate and Clean Air Coalition
- Jiunge na Cool Coalition
- Ambia meya aandae mjadala mtandaoni na wananchi ili wazungumzie masuala ya mazingira ya mjini
- Weka malengo mapya yanayohusu mazingira na bayoanuai

**Hapa kuna jinsi ambavyo miji inaweza KUCHUKUA HATUA kwa manufaa ya mazingira:**

- Tumia mbinu ya "Whole-of-Government" ili kuwezesha maono makuu ya kufikia maendeleo endelevu mjini
- Jumuisha masuluhisho yanayojali mazingira kama sehemu ya kushughulikia hali ya hewa mjini
- Buni mifumo ya usafiri inayozingatia mifumo ya ekolojia, inayotoa kivuli kwa watu wanaotembea na wanaondesha baisikeli na pikipiki na kupanda miti ndani na nje ya miji
- Weka malengo ya kutunza na kupanda miti mijini, buni sera itakayokuza ubunifu itakayowezesha upandaji wa miti huku ujenzi wa mali isiyohamishika unapoendelea
- Amua kuwa kabla ya kutoa kandarasi ya ujenzi wa nyumba za bei nafuu, ni sharti wanaotaka kandarasi waahidi kuwa watapanda mimea juu ya paa na kutumia nishati ya jua
- Toa fursa zitakazowezesha wanajamii kukuza bustani mijini
- Unda ripoti kuhusu maendeleo endelevu na isasishe mara kwa mara
- Miji yote, iwe midogo au mikubwa, inaalikwa kushiriki katika mradi huu wa kipekee ili kukuza na kuimarisha mazingira ndani na nje ya miji kote duniani. Jiunge na Cities with Nature
- Shirikisha wapangaji wa miji wachunguze jinsi miti zaidi inavyowezwa kupandwa katika maeneo ya makazi, karibu na shule na karibu na hospitali
- Iwapo maeneo asili ya maji yametumiwa wakati wa ujenzi wa miji, uliza wanaotoa mpangilio wa miji iwapo kuna uwezekano wa kuyatwaa tena
- Tenga fedha za uboreshaji wa bayoanuai katika bajeti ya kila mwaka
- Kwa ushirikiano na wanasayansi, tafiti kuhusu huduma za ekolojia unayoweza kutumia katika mji wako na uitunze na kuihifadhi

# SERIKALI ZINAWEZA KUFANYA NINI?



**Sera dhabiti na za mazingira za kujitolea ni muhimu ili kukomesha uharibifu wa bayoanuai na kutunza mazingira kwa manufaa ya maisha ya mwanadamu. Serikali zina kazi muhimu ya kufanya ili kutuwezesha kubadilisha mienendo yetu ya uharibifu na kuanza kutunza mazingira duniani kwa kutunza na kuhifadhi makazi ya wanyamapori bila kuchoka na kwa njia ya uwajibikaji. Bayoanuai ni muhimu kwa haki mbalimbali za binadamu, ikiwa ni pamoja na haki ya kuishi, haki ya afya, haki ya chakula, haki ya maji na haki ya utamaduni. Ili kulinda haki za binadamu, Majimbo yana jukumu la kutunza mifumo ya ekolojia na kutunza bayoanuai. Tukielimika zaidi, tutaimarisha juhudi zetu Kwa hivyo, ni sharti kuanza na KUJIFUNZA kuhusu yale tunayoweza kufanya; KUSHIRIKI maarifa hayo na wananchi wakati wa Siku ya Mazingira Duniani; na KUCHUKUA HATUA za kubadilisha yale tunayostahili kubadilisha.**

**Hapa kuna rasilimali zinazoweza kutumiwa na serikali KUJIFUNZA jinsi zinavyoweza kushughulikia bayoanua:**

- Mkataba wa Uanuai wa Kibayolojia unaopatikana mtandaoni unaonyesha sera za bayoanuai zilizowekwa na nchi cbd.int/countries/

- Tathmini ya Rasilimali za Misitu Duniani hutoa taarifa muhimu ya kuelewa kuhusu rasimali za misitu, hali yake, uendeshaji wake na matumizi yake fao.org/forest-resources-assessment/en/

- Haya ni maskani ya Malengo ya Maendeleo Endelevu kama sehemu ya Ajenda ya Umoja wa mataifa ya mwaka wa 2030 sustainabledevelopment.un.org/

- Mwongozo huu unaonyesha jinsi ya kutunza bayoanuai katika misitu ya maeneo ya tropiki barani Asia nap.edu/read/989/chapter/12#394

- Taarifa za kweli za UNEP zinaonyesha jinsi ambavyo majimbo yanaweza kuingiza masuala ya bayoanuai wakati wa kufanya maamuzi unenvironment.org/resources/factsheet/mainstreaming-biodiversity-information-heart-government-decision-making

- Jifahamishe zaidi kuhusu 'International Plant Protection Convention' hapa; soma mwongozo huu kupata ushauri kuhusu jinsi ya kutoa taarifa kuhusu masuala haya, na tumia rasilimali hii katika mitandao ya kijamii

- Soma ripoti hizi kuhusu matumizi ya ardhi, haki za ardhi na athari zake kwa mazingira catalogue.unccd.int/823_GLO_Full_Report_ENG.pdf catalogue.unccd.int/825_Transformative_action_brochure%20GM.pdf catalogue.unccd.int/1210_UNCCD_SPI_2019_Report_1.2.pdf

- Ripoti hii kuhusu Mkataba wa Bayoanuai ya Kibayolojia inatoa ushauri wa kisera wa kujumuisha bayoanuai na mifumo ya ekolojia

- Jifahamishe kuhusu Uendelevu, Uthabiti na Usalama (3S) na miradi ya Great Green Wall

**Hapa kuna ushauri jinsi ambavyo serikali zinaweza KUSHIRIKI malengo yake wakati wa Siku ya Mazingira Duniani:**

- Zuru mitandao ya kijamii ya UNEP kwenye sehemu ya 'feeds' kuanzia tarehe 28 mwezi wa Mei hadi tarehe 5 mwezi wa Juni na ushiriki na ulimwengu umuhimu wa kutunza mazingira. Hakikisha unatumia hashtagi #TutunzeMazingira na #SikuYaMazingiraDuniani

- Anzisha mradi wa kitaifa unaohusu bayoanuai na uonyeshe jinsi utakavyoutekeleza

- Ambia viongozi waanzishe mjadala mtandaoni kuhusu mbinu mpya za kuhifadhi mazingira wakati COVID-19 inapoendelea na uhakikishe unashiriki ujumbe huo na watu wengi

- Zungumzia masuala ya kweli mtandaoni na kupitia hotuba kuhusu bayoanuai inayopatikana katika nchi yako, na ni vipi ilivyo hatarini iwapo hatua hazitachukuliwa

- Tangaza kuwa umekomesha matumizi ya plastiki inayotumiwa mara moja tu

- Weka mikakati mipya ya kutunza maeneo ya bahari au vyanzo vya maji

- Hamasisha kuhusu mikakati mipya ya kutunza misitu, mbuga za wanyama na maeneo makuu ya bayoanuai

- Anzisha kampeni ya kitaifa ya uhamasishaji kuelimisha wananchi kuhusu bayoanuai na jinsi ya kuitunza wakati wanapoendelea na shughuli zao za kila siku ili kufikia Lengo la Kwanza la AICHI

**Hapa kuna yale ambayo serikali inaweza kufanya ili KUCHUKUA HATUA kwa manufaa ya mazingira:**

- Kupea utunzaji wa bayoanuai kipao mbele wakati wa kufanya maamuzi na uzingatiwe wakati wa kuweka ajenda ya kitaifa

- Boresha ardhi iliyoharibiwa na kutoa zawadi ili kuwatuza wale wanaoboresha na kutumia rasilimali vizuri

- Ni sharti watunga sera wabuni na kuimarisha mifumo ya fedha (dhamana, marupurupu) na mifumo ya sheria (kuripoti au kuweka wazi) ili kusaidia na kuimarisha juhudi za sekta ya binafsi za utunzaji wa bayoanuai

- Shirikiana na watunza sera kuhusu makazi ya wanyamapori na uhifadhi wa mazingira na kutoa fedha zinazohitajika kutegemea ukadiriaji unaotolewa na watu wanaotunza mazingira ili kutunza bayoanuai

- Komesha matumizi ya nishati ya visukuku na wekeza katika nishati jadidifu na ujumuishe wale wanaofanya kazi ya nishati ya visukuku kwenye sekta ya nishati jadidifu

- Piga marufuku matumizi ya magari yanayotumia mafuta na petroli na kujitolea kutumia magari yanayotumia umeme

- Hifadhi maeneo yaliyo na mali ghafi na uweke faini kali iwapo hili halitatimizwa

- Imarisha utekelezaji wa ‘Strategic Environmental Impact Assessments’

- Baada ya COVID-19, amua kutenga masaa ambapo magari hayataruhusiwa kufanya kazi ili kuwezesha wanyamapori kutembea bila kuzuiliwa na kupunguza kelele na uchafuzi

- Shirikiana na mashirika ya Umoja wa Mataifa kukuza maendeleo endelevu na kufikia malengo kama Mkataba wa Paris na Malengo ya Maendeleo Endelevu


- Tafuta masuluhisho ya kiasili (NbS), huku ukipunguza athari mbaya za miundo msingi mibofu kwa mifumo ya ekolojia na uanuai wa kibayolojia

- Kuza lishe bora endelevu na punguza uharibifu wa chakula duniani

- Wekeza zaidi kwenye kilimo endelevu na boresha mashamba ya kilimo ili kutunza mazingira na kuwezesha uzalishaji wa chakula bora

- Tunza mali ghafi kwa njia endelevu hata wakati wa kuunda sera

# SHULE NA WAALIMU WANAWEZA KUFANYA NINI?



**Shule na walimu wana jukumu la kipekee la kukuza vijana na kuwafanya wapende mazingira na kuandaa mitaala inayosisitiza umuhimu wa bayoanuai na kuwawezesha kuwa na hamu ya kutafuta ajira isiyochafua mazingira siku zijazo Ili kukomesha uharibifu unaoendelea na kuanza kutunza mazingira. Ni sharti tuanze na; KUJIFUNZA kuhusu tunayoweza kufanya; KUSHIRIKI maarifa hayo na jamii wakati wa Siku ya Mazingira Duniani; na KUCHUKUA HATUA za kubadilisha yale tunayostahili kubadilisha.**

**Hapa kuna rasilimali muhimu kwa wanafunzi kutumia KUJIFUNZA kuhusu jinsi wanavyoweza kutunza mazingira:**

- Shule ya 'TED-Ed Earth School' inasaidia vijana kuelewa na kujivunia dunia yetu asilia, huku wakijifundisha kuhusu jinsi tunavyoyategemea mazingira. Mafunzo muhimu kuhusu mazingira yamekusanywa na kuwekwa pamoja ed.ted.com/earth-school

- Mfuko wa Wanyamapori Duniani hutoa rasilimali kuhusu bayoanuai kwa shule za msingi, kwa shule za upili na kwa vyuo vikuu schools.wwf.ca/

- Kipindi kirefu mno, kinachoendeshwa na Balozi wa Amani wa Umoja wa Mataifa, Malala Yousafzai, kinafundisha watoto na vijana kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu vimeo.com/138852758

- Mkataba wa Uanuai wa Kibayolojia umeandalia walimu ratiba ya vipindi cbd.int/doc/bioday/2008/ibd-2008-framing-booklet-en.pdf

- The Nature Conservancy ni shirika lisilokuwa la kibiashara linalofanya kazi kuhakikisha watu na mazingira vinaishi vizuri

- Jifahamishe zaidi kuhusu Mkataba wa Kimataifa wa Utunzaji wa Mimea hapa, pitia mwongozo huu ili ufahamu jinsi unavyoweza kuzungumzia masuala haya, na utumie rasilimali hii kwenye mitandao ya kijamii

- Hii education kit itafundisha wanafunzi wako kuhusu kukabiliana na majangwa, na hii inahusu maeneo kame

- IUCN's #NatureforAll Discovery Zone vina vifaa vinavyoweza kutumiwa kwa ubunifu – inajumuisha video, maandalizi ya vipindi na vitabu vya futuhi ili kukusaidia kujifundisha kuhusu mazingira

**Hapa kuna namna unavyoweza KUSHIRIKI ujumbe huu wakati wa Siku ya Mazingira Duniani:**

- Chagua kipindi cha 'Earth School' unachokipenda zaidi na shiriki na marafiki wako kwa kutumia hashtagi#EarthSchool na #TutunzeMazingira

- Tumia sanaa kama njia ya kueneza ujumbe. Hivyo ni kusema, kupitia mashindano ya michoro mtandaoni au kupitia maonyesho au kupitia mashindano ya mziki

- Zuru mitandao ya jamii ya UNEP kwenye sehemu ya 'feeds' kwanzia tarehe 28 mwezi wa Mei hadi tarehe 5 mwezi wa Juni na ushiriki na ulimwengu umuhimu wa kutunza mazingira. Hakikisha unatumia hashtagi #EarthSchool na #SikuYaMazingiraDuniani

- Tagi watu kadhaa/mashirika/kampuni unapojibu na uwaombe washiriki kwenye majadiliano

- CITIES4FORESTS imezindua Shindano la Misitu. Shiriki katika shindano la picha na upande mti cities4forests.com/forest-challenge/

- Shule zinaweza kupiga marufuku matumizi ya plastiki zinazotumika tu mara moja

- Weka mtandaoni video ukihoji watu wa familia yako waeleze jinsi wanavyohakikisha kuwa wanatumia rasilimali kwa njia endelevu nyumbani

**Hapa kuna jinsi unavyoweza KUCHUKUA HATUA kwa manufaa ya mazingira:**

- Himiza wanafunzi watafakari kuhusu siku yao na waeleze kiwango cha plastiki wanachokutana nacho-kama mirija na chupa za plastiki za maji zinazotumika mara moja -na udharura wa kushughulikia suala hili. Waeleze jinsi wanavyoweza kuepuka kutumia plastiki zinazotumika tu mara moja

- Kuwa na siku ya kupanda miti shuleni

- Buni fursa zinazoweza kushirikisha vijana kwenye shughuli zinazohusiana na mazingira. Tenga siku moja kwa mwezi ya kushughulikia mazingira, andaa mashindano ya michezo inayofanyika nje na andaa matembezi ya kujifunza kuhusu flora na fauna

- Fundisha wanafunzi jinsi ya kujieleza kupitia kuandika barua kwa serikali ya mtaa wakiitaka kuimarisha juhudi za kutunza bayoanuai iliyo karibu na maeneo hayo

- Himiza wazazi kupitia shughuli zinazohusiana na elimu shuleni kununua bidhaa wanazoweza kutumia tena na kununua chakula kisichofungwa kwa vitu vingi

- Himiza wanafunzi kula chakula cha kutosha na wala wasiharibu chakula

- Kila siku, jumuisha vipindi vinavyohusu bayoanuai, ambapo unaweza kufundisha wanafunzi kuhusu spishi zilizo hatarini kuangamia au zile zilizo na umuhimu mkubwa. Hali hii huwafanya kutafakari kuhusu umuhimu wa wanyamapori

- Himiza wanafunzi kutafakari kuhusu utumiaji wa bidhaa na hatari yake kwa sayari

- Fundisha kuhusu fursa zinazotokana na ajira isiyochafua mazingira

# VIJANA NA MAKUNDI YA VIJANA YANAWEZA KUFANYA NINI?



**Vijana ni nguzo ya siku zijazo, na uamuzi unaofanywa sasa utaathiri hatima ya siku zijazo duniani. Kwa haraka, unaweza kusikika na hata kuleta mabadiliko. Vijana wana jukumu la kutekeleza ili kuzuia uharibifu wa bayoanuai na kutunza mazingira kwa vizazi vijavyo. Ili kukomesha uharibifu unaoendelea ni sharti tuanze na; KUJIFUNZA kuhusu yale tunayoweza kufanya; KUSHIRIKI maarifa hayo na wananchi wakati wa Siku ya Mazingira Duniani; na ikiwezekana KUCHUKUA HATUA za kubadilisha yale tunayostahili kubadilisha.**

**Hapa kuna rasilimali zinazoweza kutumiwa na vijana KUJIFUNZA kuhusu jinsi wanavyoweza kutunza mazingira:**

- GEO 6 ya vijana hutoa taarifa za kiwango cha juu za kisayansi kuhusu mazingira katika njia inayoweza kueleweka na vijana kwa urahisi unenvironment.org/resources/assessment/global-environment-outlook-6-youth
- 'Anatomy of Action' inaonyesha mambo ya dharura yanayoweza kutekelezwa na watu binafsi ili lukpunguza uzalishaji wa gesi ya ukaa anatomyofaction.org
- Jifundishe kuhusu spishi zilizohatarini kuangamia zinazouzwa kimagendo kupitia biashara haramu ya wanyamapori kupitia kampeni ya UNEP ya WildforLife wildfor.life/learn
- Kundi la UNEP la 'Major Group for Children and Youth' linajumuisha watu binafsi na mashirika ya vijana yanayofanya kazi kutunza mazingira na kuwezesha vijana kusikika katika mchakato wa usimamizi na uhifadhi wa mazingira www.youthenvironment.org/
- Hapa kuna Youth XChange Training kit kuhusu kutumia bidhaa vizuri unesdoc.unesco.org/ark:/48223/pf0000158700/PDF/158700eng.pdf.multi
- Mfuko wa Wanyamapori Duniani hutoa rasilimali kuhusiana na bayo-anuai kwa shule za msingi, za upili na kwa vyuo vikuu campus.wwf.ca/
- 'TED-Ed Earth school' husaidia vijana kuelewa na kujivunia dunia asilia, huku wakijifunza jinsi ambavyo tunaitegemea sayari yetu. ed.ted.com/earth-school
- Jifundishe kuhusu 'International Plant Protection Convention' hapa, pitia mwongozo huu upate ushauri jinsi ya kuzungumzia masuala haya, na utumie rasilimali hii katika mitandao ya kijamii.
- Soma ripoti hizi kuhusu matumizi ya ardhi, haki za ardhi na athari zake kwa mazingira catalogue.unccd.int/823_GLO_Full_Report_ENG.pdf catalogue.unccd.int/825_Transformative_action_brochure%20GM.pdf catalogue.unccd.int/1210_UNCCD_SPI_2019_Report_1.2.pdf
- Jifundishe kuhusu matumizi mazuri ya ardhi kupitia podcast hii na kifaa hiki cha elimu kilichoanzishwa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kukabiliana na Majangwa https://knowledge.unccd.int/drought-toolbox
- Gundua iwapo vipodoshi vyako vina vipande vidogovidogo vya shanga kupitia kwa apu ya Beat the Microbead beatthemicrobead.org/download-the-beat-the-microbead-app-and-take-part-in-ocean-conservation/
- IUCN's #NatureforAll Discovery Zone wana vifaa vinavyoweza kutumiwa kwa ubunifu – inajumuisha video, maandalizi ya vipindi na vitabu vya futuhi ili kukusaidia kujifundisha kuhusu mazingira

**Hapa kuna mambo ambayo mashirika ya biashara yanaweza kufanya KUSHIRIKI ujumbe huu wakati wa Siku ya Mazingira Duniani:**

- Andaa webinar au majadilano ya moja kwa moja ili kuwa na kipindi cha kuuliza na kujibu maswali kuhusu bayoanuai na kutoa masuluhisho yanayotokana na mazingira

- Tumia sanaa kueneza ujumbe huu. Unda podcast, video, mashindano ya uchoraji, mashindano ya muziki mtandaoni

- Zuru mitandao ya jamii ya UNEP kwenye sehemu ya 'feeds' kwanzia tarehe 28 mwezi wa Mei hadi tarehe 5 mwezi wa Juni na ushiriki na ulimwengu umuhimu wa kutunza mazingira. Hakikisha unatumia hashtagi #TutunzeMazingira na #SikuYaMazingiraDuniani

- Tagi watu kadhaa/mashirika/kampuni unapojibu na uwaombe washiriki kwenye majadiliano

- Taasisi ya Rasilimali Duniani imeanzisha Shindano la Misitu. Shiriki kwenye shindano la picha na upande mti cities4forests.com/forest-challenge/

- Wasilinaa kwa njia inayoeleweka kwa urahisi kwa kuhakikisha kuwa unatumia rasilimali za kuaminika ili kuepuka kutoa ujumbe usiokuwa wa kweli.

- Shiriki taarifa kuhusu janga la COVID-19 na jinsi linavyohusiana na bayoanuai ili kusaidia kukabiliana na taarifa zisizo za kweli

**Hapa kuna mambo ambayo makundi ya vijana yanaweza kufanya ili KUCHUKUA HATUA kwa manufaa ya mazingira**

- Andaa hafla ya upandaji wa miti, kusafisha mazingira katika jamii au pikniki ya ekolojia

- Andaa hafla, shughuli mitaani au sokoni ili kuhamasisha serikali zipunguze uharibifu wa mali ghafi

- Uliza viongozi wako kuchukua hatua dhabiti za kipekee za kutunza mazingira

- Weka malengo mapya ya kushughulikia hali ya hewa siku zijazo kwa kutoa mifano ya vijana wanaoshiriki katika utungaji wa sera za mabadiliko ya tabianchi

- Fikiria kuhusu kufanya kazi isiyochafua mazingira

- Jitolee kusafisha maeneo yaliyo karibu na wewe bila malipo

- Hamasisha watu zaidi washirikiane ili kupunguza taka na kutimia bidhaa chache

# MASHIRIKA YA URAIA YANAWEZA KUFANYA NINI?



**Kama mashirika ya uraia tuna jukumu la kutekeleza ili kuzuia uharibifu wa bayoanuai na kutunza mazingira kwa ajili ya siku zijazo. Ili kukomesha uharibifu unaoendelea ni sharti tuanze na KUJIFUNZA kuhusu yale tunayoweza kufanya; KUSHIRIKI maarifa hayo na jamii wakati wa Siku ya Mazingira Duniani; na ikiwezekana, CHUKUA HATUA zitakazoleata mabadiliko yanayohitajika.**

**Hapa kuna rasilimali zinazoweza kutumiwa na mashirika ya uraia KUJIFUNZA kuhusu jinsi wanavyoweza kutunza mazingira:**

- Jifundishe jinsi unavyoweza kusaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kupitia kampeni ya Shirika la Umoja wa Mataifa ya 'Act Now' un.org/en/actnow/

- Jifundishe kuhusu uchafu wa plastiki kupitia kampeni ya UNEP ya Bahari Safi na unavyoathiri viumbe wa baharini cleanseas.org/

- Jifundishe kuhusu ulanguzi wa spishi zilizohatarini kuangamia zinazouzwa kimagendo kupitia biashara haramu ya wanyamapori. wildfor.life/the-campaign

- Pitia "Anatomy of Action", inayoorodhesha baadhi ya mambo ambayo mtu binafsi anaweza kufanya kupunguza uzalishaji wa gesi ya ukaa anatomyofaction.org

- Jisajili kufanya kozi mtandaoni ya masuluhisho ya kukabiliana na majanga na kufanya mazingira kuweza kukabiliana na majanga pedrr.org/education-training-courses/massive-open-online-course-mooc-on-nature-based-solutions-for-disaster-and-climate-resilience/

- Jifundishe kuhusu mwanya wa uzalishaji wa gesi ya ukaa ili kudhibiti joto duniani kuwa nyusi joto 1.5 unenvironment.org/interactive/emissions-gap-report/2019/

- Jifundishe kuhusu 'International Plant Protection Convention' hapa, soma mwongozo huu kupata ushauri kuhusu jinsi ya kutoa taarifa kuhusu masuala haya, na kutumia rasilimali hii katika mitandao ya kijami

- 'TED-Ed Earth school' husaidia vijana kuelewa na kujivunia dunia asilia, huku wakijifundisha kuhusu jinsi tunavyitegemea sayari yetu. ed.ted.com/earth-school

**Hapa kuna mambo ambayo mashirika ya biashara yanaweza kufanya KUSHIRIKI ujumbe huu wakati wa Siku ya Mazingira Duniani:**

- Zuru mitandao ya jamii ya UNEP kwenye sehemu ya 'feeds' kwanzia tarehe 28 mwezi wa Mei hadi tarehe 5 mwezi wa Juni na ushiriki na ulimwengu umuhimu wa kutunza mazingira. Hakikisha unatumia hashtagi #TutunzeMazingira na #SikuYaMazingiraDuniani

- Tagi watu kadhaa/mashirika/kampuni unapojibu na uwaombe washiriki kwenye majadiliano

- Taasisi ya Rasilimali Duniani imeanzisha Shindano la Misitu. Shiriki katika shindano la picha na upande miti cities4forests.com/forest-challenge/

- Wasiliana kwa njia inayoeleweka kwa urahisi kwa kuhakikisha kuwa unatumia rasilimali za kuaminika ili kuepuka kutoa ujumbe usiokuwa wa kweli.

- Andaa hafla ya kuchanga pesa za kutumia kwa shughuli za mazin-

gira mahali unakotoka ili kuwezesha waumini kushiriki

- Sisitiza kuhusu hatua utakazochukua zitakazoleta mabadiliko ya kudumu wakati hali ya kawaida itakaporudi na ushauri wenzako kufaya vivyo hivyo
- Shiriki taarifa kuhusiana na janga la COVID-19 na uonyeshe uhusiano wake na uharibifu wa bayoanuai ili kukabiliana na taarifa zisizo za kweli
- Shirikiana na shirika la kijamii linalozalisha nishati jadidifu ili kuwezesha waumini kununua kwa bei nafuu na kuwashawishi kununua
- Shirikiana na duka la jumla lililo karibu nawe ili ukusanye vyakula vinavyoelekea kuharibika na kuwapa maskini bila malipo
- Tumia sanaa kama njia ya kueneza ujumbe. Hivyo ni kusema, kupitia mashindano ya michoro mtandaoni au kupitia maonyesho au kupitia mashindano ya muziki

**Hapa kuna yale mashirika ya uraia yanaweza kufanya ili KUCHUKUA HATUA kwa manufaa ya mazingira:**

- Sambaza miche ya kiasili kwa wenzako wakati mnapokusanyika
- Tenga taka na utumie taka kuunda mbolea
- Shiriki katika mijadala na makongamano kuhusu mazingira yanayoandaliwa na serikali na mashirika ya kimataifa
- Sisitiza umuhimu wa "kujiimarisha" baada ya COVID-19 huku mazingira yakipewa kipao mbele wakati wa kufanya uamuzi
- Hamasisha watu zaidi washirikiane ili kutoharibu chakula na kutumia chakula kichache
- Kuza utamaduni wa kutumia lishe bora, ikiwa ni pamoja na kupunguza ulaji wa nyama na kuhimiza ulaji wa vyakula vinginevyo
- Shawishi mashirika kuwa na maeneo yanayotunzwa
- Himiza watu kupanda miti wakati wa mikutano,
- Uliza viongozi wako kuchukua hatua dhabiti za kipekee za kutunza mazingira
- Toa mifano ya mashirika ya uraia yanayoshiriki katika utungaji wa sera za mabadiliko ya tabianchi

## MAONI YAKO NI MUHIMU

**Ni sharti jamii zote za kimataifa ziungane ili kukabiliana na uharibifu wa bayoanuai na uharibifu wa mifumo ya ekolojia. Tunawashukuru kwa kutusaidia kueneza ujumbe huu muhimu unaopatikana hapa. Tunawapongeza wote wanaojiunga nasi wakati wa Siku ya Mazingira Duniani**

**Tonaomba utoe maoni yako kuhusu mwongozo huu. Je, ni muhimu? Unaweza kuushiriki na wengine? Tunaweza kuuimarisha vipi? Tafadhali wasiliana nasi kupitia worldenvironmentday@un.org**

**Pokea shukrani kutika kwa kila mtu anayefanya kazi na UNEP.**

# TIME FOR NATURE

COLOMBIA
2020
BIODIVERSITY

WORLD ENVIRONMENT DAY

UN environment programme